
GOLDLITE ONLINE EDUCATIONAL SERVICES

KCSE SMARTFOCUS QUICK REVISION SERIES




# KARATASI YA KWANZA

# MSURURU 1-34




**2025 EDITION**

**FOR MARKING SCHEMES INBOX 0724351706 or visit our website**

**www.goldlitekcserevision.co.ke**

**MTIHANI 1**

**1.** Waziri wa Afya amewaita Washikadau katika Sekta ya Afya, wewe ukiwa mmoja wao, kujadili jinsi ambavyo Sekta hiyo inaweza kuimarishwa. Kama katibu, andika ***kumbukumbu*** za mkutano huo.

**2.** Jadili jinsi ambavyo nidhamu ya wanafunzi shuleni inaweza kuboreshwa.

**3.** Tunga kisa kitakachoafiki maana ya methali:

***Mwiba wa kujidunga hauambiwi pole.***

**4.** Tunga kisa kitakachoanza kwa maneno yafuatayo:

*Nilishindwa kuufanya uamuzi mara moja kuyaacha niliyokuwa nimejiingiza kwayo. Ghafla mawazo yangu yalirudi kwenye dhiki nilizopitia kutokana na yayo hayo niliyoingilia…*

**MTIHANI 2**

1. Wewe ni katibu katika Wizara ya Usalama. Andika ***kumbukumbu*** za mkutano ulioandaliwa kujadili athari za janga la mafuriko na jinsi ya kupambana na swala hili.
2. Ukiwa Kiranja Mkuu shuleni mwenu, andika ***memo*** kwa wanafunzi wote ukiwafahamisha umuhimu wa wanafunzi kushiriki katika mijadala inayoandaliwa shuleni.
3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana na matumizi ya methali:

   Atanagaye na jua, hujua
4. Andika kisa kinachanzia na maneno yafuatayo;

   Nilirauka asubuhi na mapema nikiwa na mseto wa mawazo, niling'amua kuwa siku ya siku ilikuwa imewadia …

**MTIHANI 3**

1. Wewe ni mkuu wa Baraza la Wanafunzi shuleni mwenu. Kumekuwa na visa vya wanafunzi kukiuka sheria za shule. Andika ***kumbukumbu*** za mkutano wa Baraza uliofanyika kujadili suala hili.
2. Jadili maafa ya mafuriko hapa nchini.
3. Andika insha inayoafiki methali**: Mti mkuu ukigwa, wana wa ndege huyumba.**
4. Andika insha itakayomalizika kwa maneno haya:

… Niliyakumbuka maneno ya mwalimu mkuu, machozi yalinitoka njia mbilimbili. Hayawi hayawi huwa.

**MTIHANI 4**

**1.** Wewe ni katibu wa Shirika la Umoja wa Vijana Kudumisha Mazingira. Mmekuwa na kikao kujadili hatua ambazo zimechukuliwa kuhifadhi mazingira nchini. Andika ***kumbukumbu*** za mkutano huo.

**2.** Mitandao ya kijamii ina faida nyingi. Jadili

**3.** Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo:

**4.** "Mkono mmoja hauchinji ng'ombe.

*Andika insha itakayoanza kwa :*

Nilipomtazama tu, alishusha uso wake kutokana na maovu aliyonitendea…

**MTIHANI 5**

1. **LAZIMA**

   Kutokea kwa mafuriko nchini kumechochewa na ukosefu wa mikakati endelevu ya kuhifadhi mazingira.Wewe ni mhariri wa **Gazeti la Mwangaza**. Andika ***tahariri*** huku ukipendekeza hatua zinazoweza kuchukuliwa ili kukabiliana na changamoto hii.
2. Matokeo ya mtihani wa kitaifa katika masomo ya Kiswahili na Kiingereza yamekuwa yakidorora kote nchini. Wewe ni mwanahabari wa nyanjani. Umepata nafasi kumhoji mkuu wa Idara ya Lugha katika Shule ya Hekima kuhusu mikakati ambayo imewekwa ili kurekebisha hali hii. Andika ***mahojiano*** hayo.
3. Tunga kisa kinachodhihirisha maana ya methali ifuatayo:

   Maji yakimwagika hayazoleki.
4. Andika insha itakayomalizikia kwa …nilitazama nyuma iliyojawa na giza totoro, nikabaini kwamba kama sio ushirikiano wa dhati, nafsi zetu zingetuama katika bahari isiyo na kina.

**MTIHANI 6**

1. Wewe ni katibu wa chama cha walinda Mazingira wasio na mipaka shuleni mwenu. Andika ***kumbukumbu*** za mkutano uliofanyika kujadili athari za mafuriko yaliyokumba eneo lenu.
2. Kumekuwa na visa vingi vya ajali za barabarani nchini. Ukiwa mhariri wa gazeti la Darubini. Andika ***tahariri*** kuhusu chanzo cha ajali hizi huku ukionyesha mikakati inayofaa kuzuia ajali nchini.
3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo:

   *Pele hupewa msi kucha.*
4. Tunga kisa kitakachomalizika kwa maneno yafuatayo: *Sikuupa moyo wangu nafasi ya kujutia niliyoyatenda. Nilikuwa nimeamua kuyajenga maisha yangu upya.*

**MTIHANI 7**

1. Umealikwa kuwa mgeni wa heshima katika hafla ya kuadhimisha siku ya mazingira. Andika ***hotuba*** utakayowatolea washiriki kuhusu **namna mbalimbali za kuhifadhi mazingira shuleni**.
2. Jadili **namna mbalimbali za kuboresha kilimo nchini.**
3. Tunga kisa kitakachoafiki maana ya methali ifuatayo: **Mui huwa mwema**.
4. Tunga kisa kitakachomalizikia kwa maneno yafuatayo: ... **Hapo ndipo nilipotambua kuwa mtu akitia bidii katika jambo fulani, atafaulu**.

**MTIHANI 8**

1. **Lazima**

   Umealikwa kuwa mgeni wa heshima katika hafla ya kuadhimisha siku ya mazingira. Andika **hotuba** utakayowatolea washiriki kuhusu **namna mbalimbali za kuhifadhi mazingira shuleni**.
2. Jadili **namna mbalimbali za kuboresha kilimo nchini.**
3. Tunga kisa kitakachoafiki maana ya methali ifuatayo: **Mui huwa mwema**.
4. Tunga kisa kitakachomalizikia kwa maneno yafuatayo: ... **Hapo ndipo nilipotambua kuwa mtu akitia bidii katika jambo fulani, atafaulu**.

**MTIHANI 9**

1. **Lazima**

   Umepata mwaliko kuwa hatibu mkuu katika kongamano la kutafuta mbinu za kuwasaidia wanafunzi wanaobaleghe kudhibiti hisia zao kwa njia mwafaka. Andika ***hotuba*** utakayoitoa.
2. Wewe ni katibu wa chama cha Walinda Amani shuleni mwenu. Andika kumbukumbu za mkutano uliofanyika kujadili namna vijana wanavyoimarisha umoja na mshikamano wa kitaifa.
3. Andika kisa kinachoafiki maana ya methali: Kila mchezea wembe, hukata vyanda vyake.
4. Andika kisa kitakachomalizika kwa maneno haya:

   .......Nashukuru sana kwa wema wako. Ufanisi tunaouona kwa mwanetu leo hii, chanzo chake ni wewe Mwangeka.

**MTIHANI 10**

1. Siku za hivi karibuni umesoma riwaya mpya iliyoandikwa na Msanifu Kombo inayoitwa : Afrika imelaaniwa. Andika ***tahakiki*** ya riwaya hii.
2. Hatua ya serikali kuu kumpa kila mwanafunzi wa darasa la kwanza tarakilishi ni manufaa sana. Jadili
3. Andika kisa kitakachodihirisha ukweli wa methali ifuatayo:

   *Ukiona cha mwenzako kikinyolewa na chako tia maji*
4. Andika insha itakayomalizikia kwa kauli hii: *Ama kweli sikufikiria wala kutegemea kuwa aushi yangu ingebadilika jinsi hiyo.*

**MTIHANI 11**

1. Wewe ni mwanaharakati wa kutetea haki za watoto. Wahutubie wanafunzi wa shule ya Uzalendo kuhusu la vyanzo vya mimba za mapema miongoni mwa watoto wa kike.
2. Wewe ni mwenyekiti wa jopo kazi lililoteuliwa kuchunguza kiini cha kupanda kwa gharama ya Maisha na jinsi serikali inaweza kusuluhisha swala hili. Tayarisha ***ripoti*** hii.
3. Andika kisa kinachoafiki maana ya methali ifuatayo : *Fahali wawili wapiganapo nyasi ndizo ziumiazo.*
4. Andika insha utakayoanza kwa maneno yafuatayo:

   *Walipofungua mlango huo, wengi hawakuweza kuzuia hisia zao. Walitoa kwi! Kwi! kwa maafa waliyoshuhudia…*

**MTIHANI 12**

1. Wewe ni katibu wa Chama cha Afya shuleni mwenu na mmekuwa na mkutano wa kujadili vyanzo vya ajali nyingi barabarani pamoja na suluhu. Andika ***kumbukumbu*** za mkutano huo.
2. Usafiri wa pikipiki za bodaboda una manufaa zaidi kuliko hasara. Jadili
3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo: Mgaagaa na upwa hali wali mkavu.
4. Tunga kisa kitakachomalizika kwa maneno haya:

..... *niliduwaa, nikasimama kisha nikaangalia nyuma huku machozi yakinitoka.Nilikumbuka wosia wa walimu na wazazi lakini tayari kitumbua kilikuwa kimeingia mchanga.*

**MTIHANI 13**

1. Vijana wengi wamejihusisha na unywaji wa vileo mitaani. Mkutano umeandaliwa kujadili mambo yanayochangia vijana hawa kujiingiza kwenye tabia hii. Andaa ***tahariri*** kwenye Gazeti ya Nipashe ukiangazia mambo hayo na upendekeze suluhisho.
2. Matatizo yanayokumba bara la Afrika ni ya kujitakia. Eleza.
3. Andika kisa kinachoafiki maana ya methali: kila mchezea wembe, hukata vyanda vyake.
4. Andika kisa kitakachomalizika kwa maneno haya:

   Nashukuru sana kwa wema wako. Ufanisi tunaouona kwa mwanetu leo hii, chanzo chake ni wewe Fatuma.

**MTIHANI 14**

1. Wewe ni katibu wa chama cha maskauti shuleni mwenu. Juma lililopita, chama chenu kiliandaa kongamano la kitaifa la masakauti nchini. Umeamua kumwandikia mwalimu mkuu kuhusu shughulizenu katika kongamano hili. Iandike **ripoti** hiyo.
2. Mwaka uliopita, rais aliongoza nchi katika kuadhimisha siku kuu ya upanzi wa miti nchini. Eleza umuhimu wa upandaji miti katika nchi yetu.
3. Andika kisa kinachosheheni maana ya methali ‘ binadamu ni mgamba hakosi la kuamba’.
4. Andika kisa kitakachoishia kwa:*“Aha, Kumbe muungwana akivuliwa nguo huchutama. Sitaisahau siku hiyo kwani sijawahi kufedheheka maishani kama nilivyoaibika siku hiyo.*

**MTIHANI 15**

1. Katika eneo la Tujikaze kumekuwa na ongezeko la visa vya udanganyifu katika mtihani ya kitaifa. Wewe ni katibu wa jopokazi lililoteuliwa kuchunguza sababu au chanzo cha visa hivyo. Andika ***ripoti*** ya uchunguzi huo huku ukitoa mapendekezo.
2. Serikali inafanya mikakati kabambe ili kupigana na janga la njaa nchini. Jadili
3. Tunga Kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo

   ***Usipoziba ufa utajenga ukuta***
4. Andika kisa kitakachomalizika kwa maneno yafuatayo:*Siku hiyo itabakia kwenye kumbukumbu zangu daima dawamu.Ilikuwa ni siku ambayo nilifedheheshwa mbele ya wandani wenzangu shuleni. Waswahili hawakukosea waliponena kuwa mwungwana akivuliwa nguo huchutama.*

**MTIHANI 16**

1. LazimaWewe ni mwenyekiti wa jopo la kuchunguza mfumko wa bei za bidhaa muhimu nchini na jinsi serikali inaweza kusuluhisha tataizo hili.Tayarisha ***ripoti.*** (alama 20)
2. Suala la Afya ya akili halijapewa umakini ufaao katika jamii. Angazia baadhi ya vyanzo vya changamoto hii na athari zake katika jamii. (alama20)
3. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: (alama 20)

   *Aso hadhari ni ng’ombe.*
4. Andika kisa kitakachomalizika kwa kauli ifuatayo: (alama 20)

…ndio sasa nimetambua ,mahusiano chanya ni mhimili katika ujenzi wa jamii.

**MTIHANI 17**

1. Wewe ni chifu wa kata ya Mwangaza. Umeandaa mkutano wa wanakata wako. Andika ***hotuba*** utakayotoa kuhusu mambo yanayoathiri utangamano wa kitaifa na hatua zinazoweza kuchukuliwa.
2. Mitandao ya kijamii imechangia pakubwa utovu wa nidhamu shuleni. Jadili.
3. Andika kisa kinachodhihirisha maana ya methali; ***Ukicheza ujanani utalipa uzeeni***
4. Endeleza kisa kifuatacho. ***Niligutuka ghafula, nikashangaa ni jambo lipi limenikataza usingiziwangu wa pono. Ndipo nikasikia mayowe kutoka kwa jirani. Nikakurupuka na kutoka nje mbio. Kumulika kwa jirani, nyumba yake haikuwa inaonekana…………***

**MTIHANI 18**

1. Wewe ni katibu wa kamati inayoshughulikia namna ya kupunguza kiwango cha umaskini nchini Poromoka. Andika ***kumbukumbu*** za mkutano wenu wa tatu katika mwaka huu.
2. Mfumo mpya wa elimu ya umilisi ndio suluhu kwa matatizo mengi nchini Kenya. Jadili
3. Andika insha itakayothibitisha maana ya methali hii:
   *Asiyekubali kushindwa si mshindani.*
4. Tunga kisa kinachoanza kwa maneno yafuatayo:
   Siku nyingi zilikuwa zimepita na bado sikujua alikokuwa baba yangu…

**MTIHANI 19**

1. Wewe ni mwalimu mkuu wa Shule ya Upili ya Twajitahidi. Katika shule hii wanafunzi wana matatizo tele. Waandikie walimu wako ***memo*** ukiwaarifu kuhusu shida hizo huku ukipendekeza suluhisho.
2. Kuna njia nyingi za kuimarisha uchumi nchini Kenya. Jadili
3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo:
   *Mvumilivu hula mbivu*
4. Andika kisa kitakachomalizika kwa maneno yafuatayo:
   *…Hapo ndipo nilipofahamu kuwa ushirika huleta ufanisi. Tatizo lililowakumba Wanamotopeni kwa miaka na mikaka lilitiwa katika kaburi la sahau. Walionena kuwa umoja ni nguvu waligonga ndipo.*

**MTIHANI 20**

1. **Lazima**

Wewe ni katibu wa kamati ya maendeleo katika kaunti yenu. Andika ***barua*** kwa Gavana wa kaunti yenu ukipendekeza miradi ya maendeleo ambayo ungetaka ashughulikie katika kaunti hiyo.

2. Eleza hatua zinazopaswa kuchukuliwa kukabiliana na ongezeko la ajali barabarani.
3. Mti mkuu ukigwa wana wa ndege huyumba
4. Andika insha itayomalizika kwa maneno haya:

*……………..nilisimama nikaangalia nyuma, machozi yakanitoka njia mbilimbili nilipokumbuka wosia wa walimu, wazazi na wenzangu.*

**MTIHANI 21**

1) Wewe ni chifu wa Kata ya Mwangaza. Umeandaa mkutano wa wanakata wako. Andika hotuba utakayo toa kuhusu mambo yanayoathiri utangamano wa kitaifa na hatua zinazoweza kuchukuliwa.
2) Fafanua hatua ambazo zimechukuliwa nchini ili kukabiliana na tatizo la unyanyasaji wa jinsia ya kike.
3) Andika insha itakayo dhihirisha maana ya methali hii.

***Ukicheza ujanani utalipa uzeeni***

4) Andika kisa kitakacho malizikia kwa maneno yafuatayo.

...sasa ninaelewa maneno yake kuhusu kufanya maamuzi ya busara. Sasa nimepata baraka za wazazi na ridhaa yakuishi pamoja.

**MTIHANI 22**

1. Wewe ni mwanaharakati wa kutetea haki za watoto. Wahutubie wanafunzi wa shule ya Uzalendo kuhusu la vyanzo vya mimba za mapema miongoni mwa watoto wa kike.
2. Wewe ni mwenyekiti wa jopo kazi lililoteuliwa kuchunguza kiini cha kupanda kwa gharama ya Maisha na jinsi serikali inaweza kusuluhisha swala hili. Tayarisha ripoti hii.
3. Andika kisa kinachoafiki maana ya methali ifuatayo : *Fahali wawili wapiganapo nyasi ndizo ziumiazo.*
4. Andika insha utakayoanza kwa maneno yafuatayo:

   *Walipofungua mlango huo, wengi hawakuweza kuzuia hisia zao. Walitoa kwi! Kwi! kwa maafa waliyoshuhudia…*

**MTIHANI 23**

**1)** Wewe ni mkurugenzi wa kampuni ya chapakazi ambapo pamekuwa na visa vya ukiukaji wa maadili ya kikazi .Waandikie wafanyakazi **memo** kuwaonya dhidi ya jambo hili.

**2)** ***Utalii una faida nyingi kuliko madhara nchini Kenya***.Jadili.

**3)** Tunga kisa kitakacho bainisha maana ya methali ***Chombo cha kuzama hakina usukani.***

**4)** Tunga kisa kitaka choanza kwa maneno yafauatayo:

...........***Moyo wangu uilidunda kwa matarajio makuu.***

**MTIHANI 24**

**1.** Suala la Afya ya akili ni suala nyeti na telezi na ambalo halijapewa umakini ufaao na wanajamii kutokana na unyanyapaa unaohusishwa nalo. Ukiwa Mhariri Mkuu wa Gazeti la Mzalendo, andika **t*ahariri*** kuangazia vyanzo vya changamoto hii na kupendekeza suluhu mwafaka.

2. Vijana ndio viongozi wa kesho kama wakinasihiwa kwa njia mwafaka; kwa muda wa miaka kumi vijana wamekumbwa na matatizo chungu nzima. Onyesha matatizo haya na jinsi yananvyoweza kutatuliwa.
3. Tunga kisa kitakachodhihirisha matumizi ya methali ifuatayo: Jifya moja haliinjiki chungu.
4. Tunga kisa kitakachokamilika kwa maneno yafuatayo:

   *Kweli nimetambua kuwa, familia ni nguzo muhimu katika ujenzi wa jamii.*

**MTIHANI 25**

1. Katika eneo la Tujikaze kumekuwa na ongezeko la visa vya udanganyifu katika mtihani ya kitaifa. Wewe ni katibu wa jopokazi lililoteuliwa kuchunguza sababu au chanzo cha visa hivyo. Andika **ripoti** ya uchunguzi huo huku ukitoa mapendekezo.
2. Serikali inafanya mikakati kabambe ili kupigana na janga la njaa nchini. Jadili
3. Tunga Kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayoUsipoziba ufa utajenga ukuta
4. Andika kisa kitakachomalizika kwa maneno yafuatayo:…*Siku hiyo itabakia kwenye kumbukumbu zangu daima dawamu.Ilikuwa ni siku ambayo nilifedheheshwa mbele ya wandani wenzangu shuleni. Waswahili hawakukosea waliponena kuwa mwungwana akivuliwa nguo huchutama.*

**MTIHANI 26**

1. Gavana wa Gatuzi la Kazimoto ameng'atuliwa madarakani baada ya kashifa ya ufisadi. Ungetaka kuwania kiti hicho cha ugavana. Andika ***tawasifu*** itakayosomwa katika mkutano wa kampeni mwezi ujao.
2. Matumizi ya mihadarati ni kikwazo kikuu cha maendeleo nchini. Jadili
3. Dua la kuku halimpati mwewe. Tunga kisa kinachothibitisha ukweli wa methali hii.
4. Andika insha inayoishia kwa maneno… Kicheko kikubwa cha ghafla kilianguka ubavuni mwa Sarima. Alishtuka na kumwona mumewe katwaliwa na furaha ya ajabu.

**MTIHANI 27**

1. Wewe ni Mwenyekiti wa Tume ya kupigana na ufisadi nchini. Umealikwa kuhutubia magavana kuhusu athari za ufisadi huku ukipendekeza hatua za kukabiliana na jinamizi hili. Andika ***hotuba*** utakayoiwasilisha.
2. Mitandao ya kijamii ina madhara mengi kuliko faida. Jadili.
3. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: Achezeaye tope humrukia.
4. Andika insha itakayoanza kwa maneno yafuatayo:

   *Mara nilisikia ukemi mkali kutoka nje. Majibwa yalibweka kwa mfululizo kana kwamba yanasemezana…*

**MTIHANI 28**

1. **Swali la lazima**

   Waziri wa elimu ameteua kamati ya kuchunguza sababu zinazopeleka shule mbalimbali kutomaliza silabasi kwa wakati ufaao na mapendekezo yake.Umeteuliwa kama katibu wa kamati hiyo .Andika ***ripoti*** kuhusu suala hilo
2. Usafiri wa bodaboda umeleta madhara mengi katika jamii kuliko faida.Jadili
3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo.

   ***Kikulacho ki nguoni mwako.***
4. Andika insha itakayomalizika kwa maneno:

   ………***Aha! kumbe mwungwana akivuliwa nguo huchutama.Sitaisahau siku hiyo kwani sijawahi kufedheheka maishani kama nilivyoaibika siku hiyo.***

**MTIHANI 29**

1. Ukiwa waziri wa Elimu nchini, umealikwa kuwazungumzia wanafunzi wa Kidato cha nne katika shule ya Ufanisi. Andika ***tawasifu*** utakayowasilisha.
2. Wananchi ndio wakulaumiwa kutokana na kuzorota kwa usalama nchini Kenya. Jadili
3. Andika insha itakayoafikiana na methali *Baniani mbaya kiatu chake dawa*
4. Tunga kisa kinachomalizia maneno yafuatayo:.....*Nilijitolea kafara na msaada wangu ukazaa natija* kwa wengi.

**MTIHANI 30**

1) Andika ***tahariri*** kwa gazeti la Pambazuka ukieleza jinsi ufisadi umeathiri maendeleo ya uchumi wa taifa la Kenya.
2) ***Dhuluma dhidi ya wanawake imekita mizizi nchini***. Jadili.
3) Andika insha itakayothibithisha ukweli wa methali: ***Maji ukiyavulia nguo yaoge.***
4) Andika insha itakayomalizika kwa maneno:

… ***kwa muda mrefu nilimchukulia kama mwandani wangu wa dhati lakini haya yalinizindua.***

**MTIHANI 31**

**1.** Chamko la ugonjwa wa Korona lililemaza shughuli za michezo nchini. Wewe ni katibu wa jopokazi lililoteuliwa na Waziri wa Michezo kubuni mikakati ya kufufua michezo katika taasisi za elimu nchini. Andika ***kumbukumbu*** za mkutano huo.
2. Vijana wamekuwa wakichelea kuhusika katika mchakato wa uchaguzi. Jadili kiini cha hali hii kisha upendekeze mikakati ya kuubadili msimamo huu.
3. Tunga Kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo: Achanikaye kwenye mpini hafi njaa.
4. Andika insha itakayomalizikia kwa...*nilipotua nchini, nilishusha pumzi, nikamshukuru Jalia kwa kuponea chupuchupu katika uvamizi huo.*

**MTIHANI 32**

1. Wewe kama msimamizi wa mifumo ya elimu umealikwa na mwandishi wa habari ili kuhojiwa kuhusu changamoto zinazokumba mfumo mpya wa elimu ya umilisi. Andika ***mahojiano*** hayo.
2. Serikali za majimbo zitawafaa wananchi wote. Fafanua.
3. **Mchagua nazi hupata koroma**. Thibitisha ukweli wa methali hii.
4. Anza insha kwa maneno haya; ***Nilizinduka jimbi la kwanza na kujiandaa kwenda katika hafla…….***

**MTIHANI 33**

**1.** **Lazima :** Wewe ni waziri wa usafiri nchini. Kumekuwepo na ajali nyingi za barabarani hivyo basi umealikwa na kituo cha runinga cha Mzalendo Kufafanua sababu za ajali hizi. Andika ***mahojiano*** yenu.
2. **Ujenzi wa reli za kisasa nchini una manufaa mengi kuliko madhara**. Jadili.
3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo:**Usitukane wakunga na uzazi ungalipo.**
4. Andika kisa kinachomalizika kwa maneno yafuatayo:… **Baba niliyemfahamu kwa picha pekee, hatimaye aliwasili nyumbani baada ya miaka ishirini. Nilimkumbatia huku machozi yakitudondoka sote.**

**Kwa majibu piga simu kwa nambari 0724351706 ama tembelea tovuti www.goldlitekcserevision.co.ke**

**MTIHANI 34**

1) Wewe ni katibu wa jopo lililochunguza sababu zinazozifanya jamii mbalimbali nchini zisiwe na maridhiano na utangamano. Andika ***ripoti.***
2) Mtoto mvulana anakabiliwa na hatari ya kukosa kufaulu masomoni kuliko mtoto msichana katika karne hii. Fafanua.
3) Andika insha inayofafanua ukweli wa methali: Bila silaha usiingie vitani.
4) Andika insha itakayoanza kwa maneno yafuatayo: Sauti hiyo ilikuwa ya kutisha…